# LEARNING BY EAR 2012

## “Bado ningali mwanadamu – Riwaya inayoangazia matatizo wanayopata wauguaji wa maradhi ya akili barani Afrika”

## EPISODE 5: “Utaratibu wa matibabu”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Pendo Paul**

**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: MALEMBA AKITAKA MSAADA KUTOKA KWA MIZANJA**

- **Malemba (MKE, 35)**
- **Mizanja (MUME, 65)**
- **MSIMULIZI**

**SCENE TWO: MCHUNGAJI NA FAMILIA YA KAPAKA WAKIWA NA MTOTO MCHANGA**

- **Kapaka (MUME, 25)**
- **Cheupe (MKE, 25)**
- **MCHUNGAJI (MUME, 40)**
- **KACHANGA (SI MUIGIZAJI)**
- **MSIMULIZI**

**<u>SCENE THREE: IRENE AMPATA VALERIE NJIANI</u>**

- **Irene (MKE,19)**
- **Dora (MKE, 18)**

**<u>UTANGULIZI:</u>**

Hujambo mpenzi msikilizaji na shukran kwa kujiunga nasi katika kipindi cha **Noa bongo, Jenga maisha yako**. Hiki ni kipindi cha tano kuhusu maradhi ya akili barani Afrika kwa jina **“Bado ningali binadamu”.** Katika kipindi kilichopita, Malemba alichomewa nyumba yake na majirani zake waliojawa na ghadhabu, na kumlaumu kuwa yeye ni mchawi kwa sababu kijana wake, Chumba, aliugua maradhi ya akili. Na Kapaka, aliyetaka kujinyonga, nusra aliokolewa na bibi yake mjamzito Cheupe na mchungaji walipokuja kumuombea. Baadaye Cheupe alishikwa na uchungu wa kuzaa na kupelekwa hospitalini. Jijini, Valerie alizidi kuchanganyikiwa. Sasa anaishi kwenye majalala na tayari ashaanza kutengwa na kudhulumiwa. Usibanduke, kaa nasi kwenye kipindi hiki kipya cha leo kwa jina **“Utaratibu wa matibabu”.** Tunaanzia kijijini, ambako Malemba, akiwa hana makao, amekwenda kuomba msaada kwa mtu mmoja anayemuamini: Mizanja, mtabibu wa kienyeji.

**SCENE ONE: MALEMBA AKIMTAKA MSAADA MIZANJA**

1. **ATMO:** **AFRICAN JUNGLE AMBIENCE**

2. **MIZANJA:** Malemba, nasikitika sana kwa yale yaliotokea.

3. **MALEMBA:** Nimepoteza kila kitu, lakini nashukuru Chumba hakuwa ndani ya nyumba. Ningelimpoteza motoni.

4. **MIZANJA:** Mababa na mababu walikuwa wanamlinda.

5. **MALEMBA:** Mizanja... Nina ombi moja tu leo. Kwa vile nimepoteza kila kitu kwenye moto, sina linaloniweka hapa. Napanga kwenda jijini. Nina kaka anayefanya kazi huko na anaweza kunisaidia mimi na Chumba hadi nitakapoijenga tena nyumba yangu.

6. **MIZANJA:** Kwa hivyo, ulitaka nikupe nauli ya kwenda mjini.

7. **MALEMBA:** **(impressed)** Kweli una kipawa. Umejua shida zangu hata kabla nikujulishe!

8. **MIZANJA:** Huhitaji nguvu za kiganga kutambua hayo. Nyumba yako ilichomwa, bila shaka huna pesa. Na mjini ni mbali mno, huwezi kwenda kwa miguu ama?

9. **MALEMBA:** **(laughs)** La, sitoweza. Na hata nikiwa huko, pia nitampeleka Chumba kwa daktari. Au wasemaje?

10. **MIZANJA:** Kulialia ni woga. Unatakiwa kujiweka sawa.. kwa hivyo fanya uwezalo kumsaidia kijana wako. Ni kijana mkakamavu, nasikitika sikuweza kumsaidia. Labda wao watafaulu. Na kuhusu nyumba yako, nawajua waliokuchomea.

11. **MALEMBA:** **(surprised)** Ati? Wamaanisha nyumba yangu ilichomwa kusudi? Kwanini? Sijawahi kumkosea yeyote!

12. **MIZANJA:** Ndio, lakini wana kisasi na wewe Malemba. Wengine wao walikuja mapema na mimi nikawakanya lakini wapi. Wanakushuku kuwa wewe u mchawi.

13. **MALEMBA:** **(still shocked)** Mimi, mchawi? Siamini hilo! Mungu wangu, kwa hivyo, walitaka kuniua kwa kunichoma ndani ya nyumba yangu. Wakifikiri nilikuwa ndani.

14. **MIZANJA:** Ndio. Lakini kwa mara nyengine, mababu walikuwa wakikulinda. Ndio hata mimi naunga mkono kuondoka kwako kwa muda ili uondoshe nuksi mbaya. Hilo jambo nitalifuatilia hapa.

15. **MALEMBA:** **(starts to cry)** Sijawahi kumkosea mtu yeyote, mbona watu watake kuniua? Kwanini? Mimi namshughulikia Chumba peke yake.

16. **MIZANJA:** Kwa kweli, wengine wanaamini kuwa umemroga mwanao kwa kumsukumia mapepo. Wana mashtaka mengi kukuhusu. Lakini hayo si muhimu, nakufahamu vyema na sina shaka na najua kuwa wewe huna hatia yoyote. Ni wazi kuwa kwa sababu ya wema wako ndiyo mababu wakakuondosha kwenda kuchukua kuni ili usidhurike.

17. **MALEMBA:** **(still crying)** Lakini..lakini, mbona watu wamekuwa wanyama kiasi hiki?

18. **MIZANJA:** Tunaishi kwenye dunia katili, binti yangu. Hata hivyo, chukua hizi pesa na uanze safari yako.

19. **SFX:** **COINS JINGLING WHEN COUNTED**

20. **MALEMBA:** Mizanja, hizi ni sarafu nyingi, kwani huna noti ya pamoja?

21. **MIZANJA:** Noti hazitolewi chano mwanangu. Mtu huaguliwa na sarafu...

22. **MALEMBA:** Sikujua hilo. Mababu zako waligombana na pesa

za karatasi?

23. **MIZANJA:** La! Ni vile kuna noti za bandia siku hizi. Huwezi kughushi sarafu. Nenda sasa, na wazee na mizimu ikuongoze. Nakutakia safari njema na kila la heri.

24. **MSIMULIZI:** Mtazamo wa Kiafrika haukamiliki bila mila na desturi. Na wauguzi wa kienyeji bado wanaaminika kusaidia jamii, hususan vijijini, kunako kosekana huduma za hospitali. Mizanja, mzee mtabibu wa kiasili, pia alimfaa Malemba kwa nauli na misaada mIngine ya matibabu. Malemba alirudi nyumbani haraka baada ya kupewa msaada huo, akakusanya virago vilivyobaki pamoja na Chumba na wakaenda zao jijini. Mtu hujua atokako wala hajui aendako. Je anajua linalomsubiri huko? Lijalo halina haja ya kuchunguliwa, tutalijua sasa hivi. Sasa tummulike Kapaka ambaye mkeweke Cheupe amemletea kabinti kachanga . Wanafunzi hao wa uzazi wako nyumbani na mchungaji, lakini suala kuu tatanishi likiwa jaribio la Kapaka kutaka kujiua. Hebu tujiunge nao katika furaha na butwaa.

**<u>SCENE TWO: MCHUNGAJI NA KAPAKA WAKIWA NA MTOTO WAO MCHANGA</u>**

25. **SFX:** **NEW BORN BABY CRYING**

26. **CHEUPE:** **(faintly)** Kapaka, tafadhali nipe mtoto nimbebe, nafikiri anataka kunyonya sasa.

27. **MCHUNGAJI:** Kapaka, umesikia mke wako amekwambia nini?

28. **SFX:** **BABY KEEPS CRYING MORE AND MORE**

29. **KAPAKA:** **(screaming)** Nyamazeni! Ahh, siwezi kustahamili hizi kelele, zitanitia wazimu. Kila mtu anyamaze.

30. **SFX:** **BABY CRYING GETS LOUDER**

31. **MCHUNGAJI:** **(calms baby)** Sssshhhh…Ni sawa. Babako amechoka. Lakini yuwakupenda. Njoo totoo, malkia wangu mchanga. Oh, mtoto mzuri...

32. **SFX:** **BABY CALMS DOWN**

33. **CHEUPE:** Nashukuru, mchungaji. Tafadhali zungumza na Kapaka. Nimemstahamili vya kutosha. Sijui nifanyeje tena... hata hajaamua mtoto tutamuita nani!

34. **MCHUNGAJI:** Kapaka, Naomba twende nje kidogo kwa maongezi... hatutachukua muda mrefu.

35. **KAPAKA:** Mchungaji kwani unataka nini kutoka kwangu? Sina sadaka ya kukupa, nilifutwa kazi. Kuimba pia siwezi tena kanisani, nilipoteza sauti. Siwezi hata kuomba, nilipoteza imani. Haya la zaidi ni lipi?

36. **MCHUNGAJI:** Tafadhali, tuwape nafasi mkeo Cheupe na binti yako waliwazane. Sina ninachohitaji kwako. Naomba twende matembezi kidogo na wewe. Au huwezi kufanya hivyo?

37. **KAPAKA:** **(surprised)** Matembezi? Unamaanisha kutembea tu?

38. **MCHUNGAJI:** Hiyo tu. Tunyooshe miguu. Twende hivyo ulivyo. Tuzunguke tu angalau tupate hewa safi, itatufaa baada ya mshikemshike aliotupa Cheupe kule hospitali.

39. **KAPAKA:** Hmm. sawa, twende, lakini sitaki kuenda mbali.

40. **MCHUNGAJI:** Sawa, tutakwenda umbalu unaoutaka.

41. **MSIMULIZI:** Bila hata kujua, Kapaka alikuwa tayari yuko kwenye hatua ya kwanza katika utaratibu wa matibabu yake. Baada ya mchungaji kumshawishi Kapaka watoke nje. Usisahau, Kapaka ana siku kadhaa za kutotamani kitu, licha ya kutoka nje. Alikuwa hayuko mbali na kujitoa uhai wake. Kwengineko, Irene anamsaka kwa udi na uvumba rafiki yake Valerie. Licha ya kumtafuta kwa muda

mrefu bado hajafaulu kumtia machoni. Hata akawataarifu polisi kuhusu kupotea kwake. Lakini wapi! Hakuna anayemfananisha Valerie wa zamani na huyo wa sasa aliye majalalani. Kwa sasa, Irene anakwenda kucheza disko, angalau asahau mawazo aliyonayo kwa saa kadhaa. Alifuatana na rafikiye mwengine aitwaye Dora.

**SCENE THREE: IRENE AMPATA VALERIE NJIANI**

42. **SFX:** **WEEKEND STREET AMBIENCE AT NIGHT**

43. **DORA:** Irene, sikujua kuwa wewe ni mnenguaji hodari diskoni...

44. **IRENE:** Ah wacha zako, Dora. Ningetamani sana Valerie angelikuwa hapa pia, namtamani sana, pia najihukumu kwani sikumpa msaada wa kutosha.

45. **DORA:** Acha kujilaumu. Huwezi kumzuia mtu kuwa wazimu! Alikuwa ni lazima atakuwa wazimu kivyovyote vile, kwa hivyo achana naye na uishi maisha yako.

46. **IRENE:** Hiyo ndiyo shida, siwezi kusahau. Valerie hakuwa na ubaya wowote. Namjua, hata alikuwa mwanafunzi bora chuoni. Huoni hii ni hasara kubwa.

| | |
|---|---|
| 47. **DORA:** | La! Kwa hakika, sikumpenda. Ndiyo, inasikitisa kuwa saa hii ni wazimu kamili lakini tufanyeje? Kuna maelfu ya wendawazimu na hakuna anayewajali. |
| 48. **IRENE:** | Lakini kwanini, Dora? Kwanini tukose la kufanya katika kuwasaidia wagonjwa hawa wa akili? Wewe na mimi tunafahamu fika kuwa wengine wao wanahitaji matibabu na maangalizi tu na watarudi katika hali zao za kawaida. |
| 49. **DORA:** | Kwanini? Irene, unajua vyema kuwa tunachangamoto nyingi sana kushinda maradhi ya akili. Watu wanakufa kwa malaria, Virusi vya Ukimwi na hata kifua kikuu. Wajawazito wanaaga dunia wakati wa kujifungua watoto, vichanga vinakufa wakati vikizaliwa na mauti mengi ya aina nyengine. Unataka watu wapoteze muda kwa malengo ya kuhudumia vifo kama hivyo waangalie kutibu vichaa? |
| **50. IRENE:** | Sikupingi, Dora, zipo changamoto kemkem za kiafya. Lakini unajua nini? Ugonjwa wa akili ungelikuwa mmoja wapo. Utafiti wangu mdogo niliofanya umebashiri kuwa mmoja kati ya watu wanne wana haya matatizo. Hii ni kulingana na Shirika la Afya Duniani. Lakini unajua nini? Dunia nzima, asilimia tatu pekee ya fedha ndiyo |

imetengwa kwa ajili ya tatizo la maradhi ya akili, ilhali mfumo wa afya huhitaji asilimia 13 ili kukabiliana na maradhi haya ya akili.

**51. DORA:** **(impressed)** Shabash! Sawa basi kwani sikuwa najua hayo yote. Mmoja kati ya wanne … hao ni wengi! Hei, ukizungumza juu ya wendawazimu: mtazame yule bimdogo mwendawazimu aliyeketi pale dukani. Lazima awe mmoja kati ya hao wanne.

**52. IRENE:** Msichana yupi? Wapi?

**53. DORA:** Yule kule, hana hata nguo. Baridi lazima imemng’ata!

**54. IRENE:** **(shocked)** Mungu wangu.. Siamini macho yangu. Haiwezekani. Yule sio Valerie!

**<u>HITIMISHO:</u>**

Tukio hili la kusikitisha linafunga pazia la kipindi chetu cha tano. Kutajiri nini baada ya Irene kumuona Valerie katika hali hiyo ya kusikitisha, kusonononesha na hali ngumu? Matembezi ya Kapaka na mchungaji yatazaa matunda gani? Ni kipi kinachomsubiri Malemba na mwanae wafikapo jijini? Kwa hayo na mengineyo mengi,, utayapata katika hadithi hii ya wagonjwa wa akili barani Afrika kwa jina **“Bado ningali mwanadamu”.** Ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki tembelea wavuti wetu dw.de/lbe. Mpaka wakati mwengine, nakupa mkono wa

kwa heri.